**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI**
**SHULE YA SEKONDARI BUSHABANI**

**JINA LA MWANAFUNZI** ........................................................

**YAH: <u>MAELEKEZO NA MAHITAJI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021</u>**

Natumia fursa hii kukutaarifu kuwa mtoto wako amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari BUSHABANI iliyopo MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI baada ya kufaulu Elimu ya Msingi Mwaka 2020.

Hii ni bahati ya pekee sana hasa ukirejea kazi nzuri ya Serikali ya awamu ya Tano ya **Elimu bila malipo**, Hivyo ni matarajio yangu kwamba utatumia nafasi hii muhimu kulithibitishia Taifa, Jamii na Familia yako kwamba halikukosea kukuchagua kutoka katika wanafunzi wenzako ambao hawakupata bahati na nafasi hii muhimu

Muhula wa kwanza utaanza tarehe 11.01.2021. Hivyo utatakiwa kuripoti tarehe 11.01.2021 kwaajili ya usajili.Masomo yataanza rasimi tarehe 11.01.2021

## SARE ZA SHULE:

**WASICHANA:**

**(i)** Shati Mbili nyeupe (**polyster cotton**) mikono mifupi, shati zisiwe na mistari na zisizoonesha nguo za ndani

(ii) **Viatu vyeusi vya ngozi (2pairs)** vinavyofunika miguu na **soksi nyeupe** jozi Mbili (2)

(iii) Sketi nyeusi ndefu mpaka kwenye viatu kitambaa kiwe kizito, viatu vya raba kwa ajili ya michezo

(iv) Sketi mbili rangi ya damu ya mzee zenye rinda **nane (8)** ndefu hadi kwenye viatu.
(v) Sweta rangi ya bendera ya taifa.

**WAVULANA.**

**(i) Shati mbili nyeupe polyster cotton mikono mifupi**. Shati zisiwe na mistari na zisizoonesha nguo za ndani

(ii) Viatu vyeusi vya ngozi (2pairs) vinavyofunuka miguu visiwe vya kihuni (tough boots)
(iii) Soksi nyeusi jozi mbili na **mkanda wa ngozi.**
(iv) Bukta ya bluu, na viatu vya raba kwa ajili ya michezo.
(v) **Suruali mbili nyeusi** zenye mifuko mitatu, mfuko wa nyuma
Usiwe wa kubandika
Vi Sweta bendera ya taifa

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**(1.0) UTAMBULISHO**

(1.1) Jina la Mwanafunzi........................................................................ Jinsi...........................

(1.2) Uraia........................................................

(1.3) Mahali ulipozaliwa........................................................

(1.4) Jina la Baba............................................... Mahali alipozaliwa Baba.........................

(1.5) Jina la Mama........................................... Mahali alipozaliwa Mama........................

(1.6) Ndugu wengine (walezi). Taja wanne (4)

(i)..........................................................................................

(ii)........................................................................................

(iii)......................................................................................

(iv)......................................................................................

**(2.0) AHADI/MKATABA.**

Ninaahidi kuwa nitajifunza kwa bidii katika muda wote nitakaokuwa Shuleni na kufuata Ratiba ya Shule ipasavyo na kushika sheria za Shule kama zilivyoainishwa ikiwemo na kutoshiriki katika **Migomo**, **Fujo** na **Makosa ya Jinai,** **ai**dha mtu yeyote atakayeruhusiwa kunitembelea shuleni, nitamtambulisha kwa uongozi wa shule bila kudanganya.

**UTHIBITISHO:**

(i) Jina la Mwanafunzi........................................................................

(ii) Saini ya mwanafunzi............................tarehe...............................

**(3.0) MENGINEYO**

**3.1** Soma sheria na kanuni za shule zilizo ambatanishwa nyuma na kuelewa kwa makini,ili Kuepukana na makosa yanayoweza kukupelekea kuchukuliwa hatua za kisheria.

**3.2** "Fomu B" Fomu ya uhakiki wa **"AFYA" (FORM FOR MEDICAL EXAMINATION)** ijazwe na Daktari aliye thibitishwa na si vinginevyo.(Fomu hiyo imeambatanishwa nyuma)

**3.3** Aje na cheti cha kuzaliwa pamoja na nakala yake itakayobaki katika faili Au **" AFFIDAVIT FORM"** iliyojazwa na kuthibitishwa Mahakamani.

**3.4** Mwanafunzi na Mzazi/ Mlezi wajaze fomu ya kukubali kujiunga na shule kikamilifu. Fomu hiyo imeambatanishwa (fomu C )

3.5 Mwanafunzi ajaze fomu iliyoambatanishwa ya **" MAELEZO BINAFSI" ( Fomu C)**

3.6 Kabidhi shuleni **FOMU** zote zilizojazwa siku ya kuripoti shuleni.

***KARIBU SANA NA UJIFUNZE KWA BIDII ZOTE***

..............................................

KWIGIZE A BALTHAZAR

MKUU WA SHULE

HEAD OF SCHOOL
BUSHABANI SECONDARY SCHOOL
P O. BOX 447
KIGOMA

**VIFAA VYA KUJANAVYO SHULENI**

1.Ndoo moja ya lita 10
2.mfagio mmoja aina ya chelewa
3.mopa moja
4.Madaftari 9 counterbook na madftari 9 ya kawaida
5.Mathematical set au mkebe na kalamu

**NB: KUTOKANA NA UHABA WA MIUNDOMBINU YA SAMANI, NASHAURI KILA MWANAFUNZI AJE NA *KITI* KIMOJA NA *MEZA* MOJA KWA AJILI YA KUKALIA DARASANI.**

**FOMU A:**
Cheti cha uraia wa Tanzania (**Affidavit form**) Au nakala ya cheti cha kuzaliwa (**Photocopy of birth Certificate).** Cheti cha Uraia kijazwe na kuwekwa saini na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Wilaya au Wakili.

**FOMU B:**
Cheti cha Hospitali (kimeambatanishwa) cheti kijazwe na kutiwa saini na Mganga wa Hospitali ya Wilaya au Kituo cha Afya na Kugongwa Muhuri.
**FOMU: C** Historia ya mwanafunzi ijazwe kwenye fomu iliyoambatanishwa Fomu **C.**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**SHULE YA SEKONDARI BUSHABANI**

**SHERIA ZA SHULE.**

(1) Kila mwanafunzi ni lazima kuvaa sare ya shule wakati akiwa Shuleni na hata aendapo Nje ya shule.
(2) Ni muhimu na wajibu wa kila mwanafunzi kuwahi bila kuchelewa na kufuata Ratiba Ya Shule kuanzia asubuhi mpaka jioni.
(3) Juhudi katika kazi za mikono au Darasani na wakati wa Michezo ni wajibu wa Mwanafunzi, uzembe katika shughuli hizi hautakiwi kabisa.
(4) Kila mwanafunzi lazima aombe ruhusa anapotaka kwenda nje ya mazingira ya Shule Wakati wa Saa za Shule. Uzurulaji kwenye Masoko, Kumbi za Video,au Mitaani Hautavumiliwa hata kidogo.
(5) Kila mwanafunzi lazima ajiheshimu yeye mwenyewe na kuwaheshimu watu Wengine.
(6) Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutunza na kulinda siha ya usafi wake binafsi na Wa Mazingira yote ndani na nje ya Shule yake.
(7) Vitendo vyovyote vya kushiriki au kushawishi mgomo wa aina yoyote ni MARUFUKU kabisa.Ukiwa na shida tumia vikao au toa maoni yako ukifuata ngazi

Zilizowekwa.

(8) Ugomvi au kupigana, matusi, Lugha mbaya, utoro au kutohudhuria shuleni bila taarifa/ Kibali maalumu, kutokufanya mitihani yoyote ya shule na fujo ni MARUFUKU Shuleni.

(9) Ukiugua usijiamlie kulala nyumbani bila kutoa taarifa shuleni.

(10) Kila mwanafunzi sharti aepuke na kuchukia vitendo vya aina yoyote ya Uongo,Wizi, Uasherati, Ulevi, Uchoyo, Uvutaji sigara,Bangi, Madawa yoyote ya kulevya,kufuga Kucha, Ndevu Nywele, Kupaka rangi kucha na tabia nyingine mbaya.

(11) Kila mwanafunzi ni lazima kutunza na kulinda mali ya shule.Ukiharibu mali ya Shule Itakubidi ulipe gharama ya uharibifu huo.

(12) Upole na Utii kwa viongozi,walimu,wanafunzi wenzako na Watu wote waliokuzidi Umri ni wajibu wa kila mwanafunzi. Ubishi wenye lengo la kukwepa wajibu ni MARUFUKU kabisa.

(13) Ni MARUFUKU mvulana na Msichana kuishi chumba kimoja.

(14) **Mambo yafuatayo yanaweza kukufanya ufukuzwe Shule au Uondolewe shuleni:**

- Wizi, Uasherati, Ushoga, Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, Uvutaji Sigara,Bangi, makosa ya jinai, kupiga na kupigana.
- Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma, Picha za viongozi wa Chama Na serikali pamoja na bendera ya Taifa.
- Kudharau bendera ya Taifa.
- Kuoa au kuolewa
- Kupata Mimba, kubebesha mimba ndani na nje ya shule.
- Kutoa au Kushiriki kutoa Mimba.
- Kugoma, Kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.
- Kukataa adhabu kwa makusudi.
- Mwanafunzi kuwa na Simu ya mkononi
- Kutumia njia ambazo siyo rasmi na zimekatazwa na uongozi wa shule zinaweza kusababisha kufukuzwa shule.

(15) Kushindwa kutumia vema busara yako ni sawa na kuvunja sheria za shule.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI BUSHABANI**

..............................................

**KWIGIZE A BALTHAZAR**

**MKUU WA SHULE**

HEAD OF SCHOOL
BUSHABANI SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 447
KIGOMA